# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA KWANZA

**31 OKTOBA, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 31 OKTOBA, 2023

**I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:**

**II. DUA:**

**III. KIAPO CHA UAMINIFU:**

Mhe. Bahati Keneth Ndingo

**IV. TAARIFA YA SPIKA:**

**V. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA AFYA:**

Maelezo ya Waziri wa Afya kuhusu Azimio la Bunge juu ya Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika la Mwaka 2023 (*Treaty for Establishment of the African Medicines Agency – AMA*).

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Azimio la Bunge juu ya Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika la Mwaka 2023 (*Treaty for Establishment of the African Medicines Agency – AMA*).

**WAZIRI WA NISHATI:**

Maelezo ya Waziri wa Nishati kuhusu Azimio la Bunge juu ya Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu la Mwaka 2009 (*Statute of the International Renewable Energy Agency – IRENA*).

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge juu ya Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu la Mwaka 2009 (*Statute of the International Renewable Energy Agency – IRENA*).

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2023 [*The Written*

*Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2023*].

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 [*The Legal Sector Laws* (*Miscellaneous Amendments) Bill, 2023].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu:-

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2023 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023*].

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 [*The Legal Sector Laws* (*Miscellaneous Amendments) Bill, 2023].*

## VI. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**1. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, upi mkakati wa Serikali kufanya Marekebisho ya Sheria No. 9 ya Mwaka 2010 ya Watu Wenye Ulemavu.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**2. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Zahanati katika Kata ya Binza - Maswa.

**3. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka Watumishi, Vifaa Tiba na Tendanishi kwenye Vituo vya Afya na Zahanati katika Jimbo la Lupembe.

**4. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha kukamilisha ujenzi wa majengo ya Zahanati Kijiji cha Masagalu *Mission* - Kilindi.

**5. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Jengo la Mama na Mtoto kwenye Kituo cha Afya - Loliondo.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**6. MHESHIMIWA ALI JUMA MOHAMED (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, kuna nchi ngapi zimefungua Ofisi ndogo za Ubalozi Zanzibar.

**WIZARA YA MAJI:**

**7. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO (BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatekeleza Mradi wa Maji wa Darakuta – Magugu - Mwada hadi Minjingu - Babati.

**8. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa kupeleka maji Kata sita za Izimbya, Kyaitoke, Mugajwale, Ruhunga, Katoro na Kaibanja kutoka Ziwa Ikimba utaanza.

**WIZARA YA UJENZI:**

**9. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini *TANROADS* watalipa fidia kwa kujenga shule mbadala baada ya Shule ya Msingi Unkuku kupitiwa na Barabara ya Dodoma – Arusha.

**10. MHESHIMIWA MWATUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani kupunguza msongamano wa maroli barabarani.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**11. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKSHON SHANGAI (NGORONGORO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni Sheria ipi inawaruhusu Watumishi wa TANAPA, TAWA na NCAA kutoza Mifugo Shilingi 100,000/= pindi iingiapo Hifadhini.

**12. MHESHIMIWA OLIVER DANIEL SEMUGURUKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaona umuhimu wa kukitangaza vya kutosha Kivutio cha Maporomoko ya maji Rusumo ili kuchangia Pato la Taifa.

**WIZARA YA KILIMO:**

**13. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani wa kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la Kahawa ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kukuza soko la Kahawa.

**14. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga skimu ya umwagiliaji Kata ya Kihungu - Mbinga.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**15. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini elimu ya uvuvi, mikopo na vifaa vya kisasa vitatolewa maeneo ya Manda, Ruhuhu, Iwela, Lupingu, Lifuma, Makonde, Kilondo na Lumbila.

**WIZARA YA MADINI:**

**16. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali imefanya utafiti kuhusu uwepo wa Madini Mkoani Mtwara.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**17. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Wilaya ya Rungwe italetewa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**18. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, upi mpango wa kuboresha Vituo vya Polisi Busanda hususani Kituo cha Katoro na Chigunda.

**WIZARA YA AFYA:**

**19. MHESHIMIWA MARTHA NEHEMIA GWAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali haioni kuna haja ya Watoto wachanga kutumia Bima za Afya za Mama zao.

**VII. HOJA ZA SERIKALI:**

**MAAZIMIO:**

**WAZIRI WA AFYA:**

Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika la Mwaka 2023 (*Treaty for Establishment of the African Medicines Agency – AMA*).

**WAZIRI WA NISHATI:**

Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Tanzania Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadididifu la Mwaka 2009 (*Statute of the International Renewable Energy Agency – IRENA*).

## VIII. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023 [*The Legal Sector Laws* (*Miscellaneous Amendments) Bill, 2023].*

**DODOMA**
**31 OKTOBA, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**